***Soma kifungu kifuatacho. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Usiku ___1___ sikupata hata lepe la usingizi. Niliwaza na kuwazua kuhusu safari ___2___ kuelekea kule ___3___. Mimi na rafiki yangu ___4___ chanda na pete tulifaa kusafiri tukitumia ___5___. Asubuhi ___6___, tulijiandaa kisha tukaondoka hadi kwenye stendi. ___7___ nanga mwendo wa saa mbili kamili. Safari yetu ilikuwa ya ___8___. Tuliwasili huko mwendo wa saa sita kamili. ___9___ na mjomba wangu aliyekuwa amevaa ___10___ maridadi sana. Tuliingia garini na ___11___ vumbi lililokuwa kwenye viti kabla ya kuketi. Mjomba aliliendesha gari kwa kasi kama ___12___. Ghafla gari ___13___ liliteleza na kuugonga mti uliokuwa kando ya barabara. Kwa bahati ___14___, hakuna aliyeumia. Hapo ndipo mjomba alipogundua kuwa ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. yote | B. kucha | C. kutwa | D. moja |
| **2.** | A. ya | B. la | C. wa | D. cha |
| **3.** | A. Mombasa | B. Mombasani | C. mombasa | D. mombasani |
| **4.** | A. ya | B. wa | C. za | D. mwenye |
| **5.** | A. gari ya moshi | B. garimoshi | C. gari la moshi | D. gari na moshi |
| **6.** | A. huo | B. hilo | C. hiyo | D. hio |
| **7.** | A. Tulinoa | B. Tulitia | C. Safari iling'oa | D. Tuling'oa |
| **8.** | A. masaa manne | B. masaa nne | C. saa manne | D. saa nne |
| **9.** | A. Tulipokewa | B. Tulipokea | C. Tulipokelewa | D. Tulipokelea |
| **10.** | A. buibui | B. bulibuli | C. hijabu | D. kanga |
| **11.** | A. kupanguza | B. kupunguza | C. kuchunguza | D. kupangusa |
| **12.** | A. umeme | B. ajali | C. kobe | D. kinyonga |
| **13.** | A. yenyewe | B. enyewe | C. lenyewe | D. wenyewe |
| **14.** | A. kubwa | B. mzuri | C. mbaya | D. nzuri |
| **15.** | A. polepole ndio mwendo | | B. ajali haina kinga | |
| | C. ngojangoja huumiza matumbo | | D. adui mpende | |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua orodha ambayo ina viunganishi pekee.
A. wangu, chake, lao.
B. baada ya, kabla ya, kati ya.
C. nguo ya, gari la, kiti cha
D. bila, wala, lakini

**17.** Tambua sentensi ambayo imetumia 'ji' kuonyesha mtendaji.
A. Jibwa hili ni la polisi.
B. Unywaji wa pombe ni hatari kwa afya yako.
C. Mkulima yule amejikata kidole.
D. Mbebaji wa mawe amemaliza kazi.

**18.** Jaza nafasi kwa jibu linalofaa.
**Tulienda shambani kupalilia na ________ magugu.**
A. kung'oa B. kunyunyizia
C. kuvuna D. kupanda

19. Chagua alama ya kuakifisha ambayo ni **kikomo**.

A. ,  B. " "

C. !  D. .

20. Sentensi gani ambayo ni sahihi kati ya hizi?

A. Gari jenyewe ni jeusi.

B. Gari lenyewe ni leusi.

C. Gari lenyewe ni jeusi.

D. Gari la mwenyewe ni mweusi.

21. Gani **si** rangi ya upinde wa mvua kati ya hizi?

A. Nyekundu  B. Nili

C. Hudhurungi  D. Urujuani

22. Maneno haya yanapatikana katika ngeli gani? **'unga, ugali, uji'**

A. U - U  B. U - YA

C. U - I  D. U - ZI

23. Chagua umoja wa: **Maziwa ya watoto yamemwagika karibu na nyuzi**.

A. Ziwa la mtoto limemwagika karibu na uzi.

B. Maziwa ya mtoto yamemwagika karibu na uzi.

C. Ziwa la watoto limemwagika karibu na nyuzi.

D. Maziwa ya watoto yamemwagika karibu na uzi.

24. Jibu la **'u hali gani'** ni ________

A. sina la kuamba  B. chewa

C. njema  D. binuru

25. Udogo wa **'Mti '** ni ________

A. kiti  B. kimti

C. kamti  D. kijiti

26. Chagua sentensi ambayo imetumia kivumishi cha sifa.

A. Matunda yote yameiva.

B. Darasa la tatu lina wanafunzi wengi.

C. Chakula kitamu kitapewa mwalimu.

D. Shule yetu inajulikana kote.

27. Shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti huitwaje

A. malenga  B. takhmisa

C. tarbia  D. ngonjera

28. Kutokana na kitenzi **'andika'** tunapata nomino gani?

A. Mwandishi  B. Andikia

C. Kitabu  D. Kalamu

29. Chagua kinyume cha;

**Baba ameuza nguo nzuri.**

A. Baba hajauza nyuo nzuri.

B. Mama ameuza nguo mbaya.

C. Dada amenunua nguo mbaya.

D. Mama amenunua nguo mbaya.

30. Bunda ni la noti, nao mwongo ni wa ________

A. kuni  B. miaka

C. nyuki  D. takataka

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.</u>***

Inajulikana kabisa kuwa nyumba imara hujengwa kwa mchanganyiko wa vitu vingi. Vitu hivyo ni kama vile mawe, simiti, mchanga, kokoto na kadhalika. Je, mwili wako nao unajengwa na nini? Mwili wa binadamu hujengwa kwa chakula. Chakula hicho ni lazima kiwe chakula bora na mlo kamili. Mlo kamili unajumuisha makundi matatu ya vyakula ambayo ni: nafaka, mizizi na ndizi, kundi la pili ni la vyakula vyenye jamii ya kunde na vyenye asili ya wanyama, kundi la tatu ni la mbogamboga, kundi la nne ni la matunda nalo kundi la tano ni la mafuta na sukari.

Mwili unahitaji chakula chenye mchanganyiko wa makundi haya ya chakula ili kuwa na afya bora na iliyo imara kama inavyolinganishwa na nyumba imara. Chakula kikiwa hakina au kina kiwango kidogo cha baadhi ya makundi ya chakula yaliyotajwa hapo juu lazima mwili utakuwa dhaifu, hata mwili huo hautakua vizuri. Magonjwa yatokanayo na utapiamlo ndio chanzo kikuu cha mwili kuwa na afya mbaya. Utapiamlo hutokana na lishe duni.

Lishe duni ni hali ya mwili kukosa virutubishi vinavyohitajika mwilini. Virutubishi hivi ni kama vile protini, wanga, mafuta, vitamini na madini. mwili ukikosa baadhi ya virutubishi hivi

hushindwa kufanya kazi vizuri. Hali hii husababisha madhara mengine mengi. Magonjwa ya utapiamlo ni kama vile kwashakoo, upungufu wa damu, ukosefu au upungufu wa vitamini na kadhalika. Ni vyema kula vyakula vyenye mchanganyiko wa kila kundi la chakula ili uwe na afya nzuri. Pia ukila lishe bora hutapatwa na maradhi mara kwa mara. Unafaa kunywa maji safi na salama wakati wote unapohitaji.

**31.** Ni gani kati ya vitu vifuatavyo hutumika kujenga nyumba lakini hakijatajwa katika aya ya kwanza?

A. Mbao B. Simiti
C. Mchanga D. Mawe

**32.** Ni nini ambacho kimelinganishwa na nyumba katika ufahamu?

A. Chakula B. Kujenga
C. Mwili D. Mbao

**33.** Mlo kamili unajumuisha makundi mangapi ya vyakula?

A. 1 B. 3 C. 5 D. 4

**34.** Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa:

A. nyumba ya binadamu hujengwa kwa chakula
B. nyumba imara hujengwa kwa mchanganyiko wa vitu vitano
C. mwili wa binadamu hujengwa kwa chakula
D. maji si muhimu kwa mwili wa binadamu.

**35.** Chakula gani ambacho hakipatikani katika kundi la nne?

A. Sukumawiki B. Maembe
C. Machungwa D. Mananasi

**36.** Kulingana na aya ya pili, ni kweli kuwa:

A. mwili unahitaji kundi moja tu la vyakula ili kuwa imara.
B. mtu akila chakula kidogo, mwili wake utakuwa dhaifu.
C. afya mbaya huletwa na magonjwa yatokanayo na utapiamlo.
D. utapiamlo hutokana na lishe bora.

**37.** Ni kweli kwamba lishe duni ni;

A. hali ya mwili kukosa protini
B. hali ya mwili kukosa virutubishi vinavyohitajika
C. hali ya kuishi bila magonjwa
D. hali ya chakula kukosa protini.

**38.** Upi si ugonjwa wa utapiamlo kulingana na ufahamu?

A. Kichocho.
B. Kwashakoo.
C. Upungufu wa damu.
D. Upungufu wa vitamini.

**39.** Ili uwe na afya bora, ni vyema ufanye nini kulingana na aya ya mwisho?

A. Uishi katika mazingira yaliyo safi.
B. Uoge kila wakati
C. Unywe maji ambayo si safi.
D. Ule vyakula vyenye mchanganyiko wa kila kundi la chakula.

**40.** Mwandishi anaeleza kuwa ukila lishe bora:

A. utapatwa na maradhi mara kwa mara
B. hutapatwa na maradhi
C. huwezi ukafa
D. hutapatwa na magonjwa kila wakati.

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.</u>***

Siku moja tulitangaziwa kuwa tungekuwa na sherehe ya kuwatuza wanafunzi waliofanya vizuri shuleni. Kila mwanafunzi alijawa na furaha tele. Kabla ya siku yenyewe kufika, tulifyeka nyasi na kuokota takataka kote shuleni. Kisha tuliambiwa na mwalimu wetu wa mazingira kwamba tusizichome takataka hizo bali tuzitupe katika jalala. Baadaye tulinyunyiza maji mahali palipokuwa na vumbi kisha tukafagia. Mahema yalipangwa kisha viti vikawekwa vizuri ndani ya mahema hayo.

Mwalimu alituagiza kuwa turudi shuleni kesho yake tukiwa na nguo ambazo ni **safi kama**

**msahafu**. Keshoye tuliwasili shuleni asubuhi na mapema. Sherehe ilianza mwendo wa saa nne asubuhi. Tuliimba wimbo wa taifa kisha tukamsifu Mungu kabla ya kuketi. Mwalimu mkuu alitoa hotuba fupi na kueleza kuwa tofauti na miaka mingine, tuzo za mwaka huo zisingekuwa za masomo pekee. Pia pangekuwa na tuzo za viwango vingine.

Wanafunzi waliofanya vyema masomoni walipewa zawadi zao. Hao walikuwa wanafunzi watatu bora katika gredi ya Kwanza hadi ya nne na kisha darasa la tano hadi la nane. Pia kulikua na kiwango cha mwanafunzi aliyekuwa safi kushinda wengine wote. Hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja katika kila darasa na kila Gredi. Nilishangaa niliposikia jina langu likitajwa. Nilikuwa mmoja kati ya wanafunzi wanane waliokuwa na heshima na nidhamu. Mimi niliwakilisha wanafunzi wote wa darasa la sita. Nilijawa na furaha sana. Niliporudi nyumbani na kufungua zawadi niliyopewa, nilifurahi mno kwa kuwa nilikuwa nimenunuliwa shati zuri sana. Hakika, hiyo ilikuwa siku ya furaha sana.

---

**41.** Sherehe iliyotangazwa ilikuwa ya nini?
- A. Kuwatuza wanafunzi waliopita mtihani.
- B. Kuwatuza wanafunzi wenye bidii.
- C. Kuwatuza wanafunzi wenye nidhamu.
- D. Kuwatuza wanafunzi waliofanya vizuri shuleni.

**42.** Unadhani kwa nini wanafunzi walishauriwa wasizichome takataka?
- A. Zilikuwa haziwezi kuchomeka.
- B. Hawakuwa na mahali pa kuzichomea.
- C. Hawakufaa kuchafua mazingiwa kwa moshi.
- D. Mwalimu hakutaka wachome takataka.

**43.** Maneno '**safi kama msahafu**' ni mfano wa;
- A. tashbihi
- B. methali
- C. nahau
- D. fumbo

**44.** Sherehe ilianza saa ngapi kulingana na ufahamu?
- A. 10:00
- B. 4:00
- C. 10:30
- D. 4:30

**45.** Mwalimu mkuu alieleza kuwa tuzo za mwaka huo zingekuwaje?
- A. Zingekuwa za masomo pekee.
- B. Zingetolewa kwa walimu pia.
- C. Zingekuwa za masomo na viwango vingine.
- D. Zingetolewa kwa wazazi pekee.

**46.** Katika kiwango cha masomo, wanafunzi waliopewa zawadi katika kila darasa walikuwa wangapi?
- A. 2
- B. 3
- C. 4
- D. 5

**47.** Kwa nini msemaji alishangaa aliposikia jina lake likitajwa?
- A. Hakutarajia kupewa zawadi.
- B. Alikuwa amelala.
- C. Alikuwa mwenye tabia mbaya.
- D. Hakulijua jina lake.

**48.** Mwandishi wa kisa hiki alikuwa katika darasa lipi?
- A. 3
- B. 4
- C. 5
- D. 6

**49.** Ni nini ambacho wanafunzi **hawakufanya** kabla ya siku ya sherehe?
- A. Kufyeka nyasi.
- B. Kunyunyiza maji na kufagia.
- C. Kupewa zawadi.
- D. Kupanga mahema na viti.

**50.** Ni kweli kwamba msemaji wa makala haya ni;
- A. Mwalimu
- B. Mvulana
- C. Msichana
- D. Mzazi